

**HOTUBA YA KATIBU MKUU WA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI MEJA
JENERALI PROJEST RWEASIRA KATIKA MKUTANO BAINA YAKE NA
WAANDISHI WA HABARI LEO TAREHE 16 FEBRUARI 2017 KATIKA UKUMBI WA
MIKUTANO WA WIZARA**

Ndugu Waandishi wa Habari,

Mabibi na Mabwana,

Leo nimewaita kwa lengo moja la kuwapa taarifa kuhusu Watanzania wanaorejeshwa kutoka nchini Msumbiji.

Kama ambavyo mmeona leo vyombo mbalimbali vya habari vya hapa nchini vimetoa taarifa juu ya watanzania kama 187 waliorejeshwa toka nchini Msumbiji, baadhi ya Vyombo vimedai kwamba Watanzania hao baadhi yao wamepigwa au kunyang'anywa mali zao.

Kwanza nataka kusema kwamba Uhusiano kati ya Tanzania na Msumbiji ni mzuri sana na unaendelea kuimarika kila siku, hivyo ni jukumu la kila mwananchi kuhakikisha kuwa uhusiano huu wa kindugu ambao umekuwepo muda mrefu unaendela kuimarishwa na kutunzwa.

Pili watanzania hao wanaorudishwa nchini toka Msumbiji ama wameingia nchini Msumbiji bila kufuata taratibu za kisheria au baada ya kuingia kwa kufuata taratibu wamevunja sheria au taratibu za ukaazi na kufanya kazi bila vibali. Mgeni yeyote anayeishi ndani ya nchi yeyote duniani bila kufuata taratibu za kisheria za uhamiaji za nchi husika anakuwa amevunja sheria na taratibu za kiuhamiaji za nchi husika.

Hivyo kila nchi ikiwemo Msumbiji inayo haki ya kuwaondoa watu wa namna hii na kuwarudisha kwenye nchi walizotoka wengine hurudishwa na wengine hufungwa na baadae kurudishwa makwao.

Hata hivyo zoezi linalofanyika nchini Msumbiji halijawelenga watanzania pekee bali raia wote wanaoishi na kufanya kazi nchini Msumbiji bila kufuata taratibu za kisheria. Kwa hiyo jambo hili tusilikuze sana bila sababu za msingi.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Kurudishwa kwao watu au wageni ambao wanaishi au kufanya kazi kinyume na sheria na taratibu za nchi husika sio jambo geni hata Tanzania imekuwa inafanya hivyo pale inapobidi. Mathalani mwaka 2013 tulifanya Oparesheni Kimbunga huko Mkoani Kagera ambapo watu wapatao 37,000 waliokuwa wakiishi nchini kinyume na sheria za nchi waliondolewa na kurudishwa nchi walizotoka.

Aidha Tanzania inaendelea na zoezi la kuwaondoa watu wanaoishi na kufanya kazi nchini kinyume cha sheria za uhamiaji wengi wao kutoka nchini Ethiopia, Eritrea, Somalia na kwinginepo.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Natoa wito kwa Watanzania wanaotaka kwenda nchi za nje kufanya kazi , biashara au shughuli yoyote halali wafuate sheria, pia natoa wito kwa vyombo vya habari kutoa taarifa ambazo hazitachangia kuvunja mahusiano mazuri kati yetu na majirani zetu au nchi marafiki. Hatupendi kuingia kwenye mgogoro wa kisiasa au kidiplomasia na nchi ya Msumbiji ambayo tumekuwa na uhusiano mzuri tangu nchi hiyo ilipopata uhuru wake kutoka kwa Wareno mwaka 1975.

Kama kuna tatizo zipo taratibu za kidiplomasia za kulitatu lakini sio kupitia vyombo vya habari au kupiga picha. Aidha tuepuke kutoa habari ambazo zinaweza kuzua au kuchangia chuki kati ya Watanzania na watu wa nchi nyingine ambao wanaishi nchini Mwetu Kama wapo wageni wa namna hiyo basi kuna taratibu za kisheria zitafuatwa kuwaondoa na kuwarejesha makwao.

ASANTENI KWA KUNISILIKIZA.